

FURSA ZA UWEKEZAJI ZINAZOPATIKANA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO

1. VIWANDA VYA USINDIKAJI WA MAZAO YA MIFUGO

Kiteto ni moja ya maeneo pekee Tanzania yaliyojaliwa kuwa na mifugo tele, hii imepelekea kuwa kinara kwa Minada ya ndani ya Wilaya ambapo wanyama kama vile Kuku jumla wapo 141,472 Kondoo jumla wapo 161,612 Mbuzi wapo 448,106 na Ng'ombe jumla wapo 484,833 wanyama wote hawa hununuliwa kwa ajili ya nyama katika mikoa mingine hususani Dar es salaam, Dodoma, Arusha, Tanga na kwingineko hutegemea Minada ya Kiteto.

Pia uwekezaji wa Viwanda vya kusindika mazao yatokanayo na mifugo kama vile Maziwa, Ngozi, Vifungo na Nyama unafaa.



Mifugo katika Kata ya Kijungu Kiteto kushoto ni Mbuzi na kulia ni Ng'ombe

2. VIWANDA VYA USINDIKAJI WA MAZAO YA KILIMO

Kwa takwimu kwa mwaka jumla ya **tani** 155,636 za Mahindi hupatikana, Mbaazi jumla ya tani 18,358 Maharage jumla ni 1,382 na Alizeti ni 37,397. Kutokana na fursa ya upatikanaji wa Mazao ya Kilimo uwekezaji wa Viwanda vya kusindika mazao yatokanayo na kilimo kama vile unga wa sembe, mafuta ya alizeti, vyakula vya mifugo, utengenezaji wa biskuti na chokleti fursa hii inafaa sana kuwekezwa.



Kushoto ni zao la biashara la Alizeti na kulia ni zao la chakula na biashara pia Mahindi katika Kata ya Kiperesa.



Mbaazi Zao la Biashara Kata ya Kiperesa

3. UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MADINI

Kutokana na upatikanaji wa madini kama vile Rubi, Redganet, Greentormaline, Rhodelight, White quartz. Fursa hii iko wazi kwa wawekezaji kuja kuchimba madini haya.



Madini yaliyopo Kiteto ni Rubi, Redganet, Greentormaline, Rhodelight

4. UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MISITU

Kutokana na kuwepo kwa upatikanaji wa miti kama vile Mpingo, Mninga, Mtondoro, Mkindu, Mlama, Mgunga, Mpilipili na mingineyo mingi ambapo Mbao, Magogo, Mkaa, Miti ya uchongaji vinyago hupatikana hapa fursa hii ipo wazi kwa wawekezaji.

Kutokana na kuwepo kwa msitu wa SULEDO unaotambulika Kimataifa kwa kuwa na jamii ya miti na maua adimu ya aina mbalimbali imekuwa ni kivutio kwa nyuki ambao hutengeneza asali, fursa hii inaweza kuwekezwa kwa ajili ya ufugaji wa nyuki na usindikaji wa asali





Picha zote 3 ni za Msitu wa Jamii wa Hifadhi ya SULEDO unaotambulika Kimataifa ambao unamilikiwa kwa pamoja na Kata 3 yaani Sunya, Lengatei na Dongo.

5. UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA UTALII

Kwa mara nyingine tena, Wilaya yetu imejaliwa kuwa na Wanyama wengi wanaopatikana katika Hifazi za Wanyama kama vile INDEMA-WMA, MAKAME yenye ukubwa wa eneo la hekta 379,362 ambapo wanyama kama vile Swala, Fisi, Twiga, Tembo, Nyati, Nyumbu, Chui, Simba na wengine wengi wanapatikana.



Kutoka kushoto ni kundi la Simba wakiwa wamepumzika na kulia ni kundi la Pundamilia wakiwa malishoni.



Kutoka kushoto ni kundi la Simba Nyati wakiwa katika malisho yao na kulia ni Fisi

Hifadhi hii ni ya kijamii ambayo ina vitalu 4 vya uwindaji ambavyo ni Irkiushbour, Talamai, Maasai, EAST AND Maasai west-Naibourmurto.

Ukanda huu ni mashuhuri kwa utalii wa uwindaji (kwa sasa uwindaji umesimamishwa hadi tamko lingine litakapotolewa), lakini utalii wa kuangalia na kuchukua picha za wanyama unaendelea, ujenzi wa Hoteli za kisasa na Camp site unakaribishwa, wanyama adimu kabisa duniani kama vile Swala Twiga, Kanga wenye kofia juu na Choraa kwa hifadhi yetu hii wapo wengi.



Wanyama adimu kushoto ni Swala Twiga na kulia ni Choraa



Kutoka kushoto ni ndege adimu Kanga wenye kofia, Twiga, Pundamilia na Tembo

Kutokana na kuwepo kwa upatikanaji wa wanyama wengi fursa hii iko wazi katika utalii wa kuwinda (kwa sasa uwindaji umesimamishwa hadi tamko lingine litakapotolewa), utalii wa kupiga picha pamoja na ujenzi wa Hoteli za kisasa na Camp site unakaribishwa.